



Kupima

Wanawake na HIV: Vifurushi vya habari za mfululizo kwa wanawake



Utambuzi wa karibu




Matibabu



Kujitunza vizuri



Ujauzito na mimi



Huduma na Tovuti ya NSW

Njia pekee kujua

HIV ni virusi vinavyosababisha UKIMWI. Watu wengi hawafahamu wanavyo. Njia pekee tu kujua kama una HIV ni kupima damu.

Wakati mtu ana virusi vya UKIMWI, tunasema yeze ni HIV positive, yaani, ni mwathirika HIV.

Mimi ni mwanamke, kwa nini nipimwe?

Nusu ya watu wanaoishi na HIV duniani ni wanawake nchini Australia, kuna karibia wanawake 1,500 wanaoathirika na HIV. Wengine wameambukizwa na mwenzi wao, au na mwenzi wa zamani.

Vipengele vikuu vya kuambukizwa HIV kwa wanawake nchini Australia ni:

- Kufanya mapenzi na mtu kutoka nchi inapokuwa na kiwango juu cha HIV
- Kushirikiana sindano na vifaa vya kupiga sindano.

HIV inaeneza kujitia:

- Ngono bila kinga (kufanya mapenzi bila kutumia kondomu) na mtu ambaye ameathirika na HIV
- Kushirikiana sindano na vifaa vya kupiga sindano.

- Mama anaweza kumwambukiza mtoto wakati wa ujauzito, wa kuzaliwa au wa kumnyonyesha
- Upaji wa damu katika nchi kadhaa. Nchini Australia damu iliyotolewa imepimwa kwa HIV tangu mwaka 1985.

Kama ukiona una mashaka una HIV, fikiria kuhusu kupimwa. Kama ukigundua kwamba umeathirika HIV, utaweza kutunza afya yako vizuri zaidi. HIV vinaweza kudhibitishwa na matibabu na watu wengi wanawea kuisha maisha ya afya na ya shughuli. Kama wewe ni mja mzito au unapanga kuwa na mtoto, kuna njia za kufaa kupunguza hatari ya kuambukiza mtoto wako.

Kuhusu kipimo cha HIV

Kipimo cha HIV ni kipimo cha damu kinachochunguza kwa kinga cha HIV katika damu yako. Kinga kinatengenezwa na mfumo wako wa kinga ya mwili wakati unapokuwa na maambukizo au virusi. Kama tokeo la kipimo ni positive, yaani umeathirika, daktari ataomba kipimo kingine kuhakikisha tokeo hilo.

Inaweza kuchukua muda wa wiki 12 kwa mwili kutengeneza kinga. Muda huu unaitwa 'muda wa kusubiri'. Maana yake ni kwamba kama umeambukizwa karibu HIV

inaweza haitaonekani katika kipimo cha kwanza na labda utahitaji kurudia kipimo tena baada ya miezi mitatu.

Naweza kupata kipimo wapi?

Unaweza kuomba kipimo kutoka daktari wa familia, Kituo cha Uzazi wa Mpango cha NSW na wakati wengine kwa Zahanati ya Afya ya Kingono.

Daktari au muuguzi aongee nawe kuhusu tofauti kati ya HIV na UKIMWI, jinsi HIV inavyoeneza na nini itatokea unapopata matokeo ya kipimo.

Wanaweza pia kuuliza maswali ya binafsikufahamu kiwango chako cha hatari. Inaitwa 'ushauri nasaha kabla kupimwa'. Pia ni nafasi yako kuuliza maswali yoyote unayo.

Huhitaji kuamua kupimwa siku ile na unaweza kwenda miadi michache kabla ya kuamua kwako. Daktari asifanye kipimo bila ruhusa yako. Ni uchaguzi wako kupimwa au la, na unaweza kuchagua daktari unayeamini.

Matokeo yatapewa kwako uso kwa uso, kama motokeo ni umeathirika au hujaathirika. Kama matokeo yako yanaonyesha wewe umeathirika na HIV, daktari atakupa ujumbe na habari zaidi ya huduma za msaada, pamoja na huduma kwa wanawake wenyе HIV. Unaweza kupiga simu zinazoandikiwa na orodha upande wa kulia na pia kwa karatasi cha habari cha Huduma na Tovuti ya NSW.

Kuweka Usiri

Sheria inasema kwamba madaktari na wafanyakazi wengine wa afya nchini ya Australia wanahitaji kutunza usiri wako. Maana yake ni kwamba hawaruhusiwi kuzungumza habari yako ya binafsi na yejote isipokuwa unawaruhusu.

Huduma

Pia ona karatasi cha habari cha Huduma na Tovuti ya NSW

Uzazi wa Mpango wa NSW

SimuAfya

Simu:1300 658 886

SimuHabari za Afya ya Kingono cha NSW

Simubure

1800 451 624

Simu za habari za HIV

Simubure

1800 451 600

Ukihitaji mkalimani piga simu 131 450

Kusoma zaidi: fuata viungo au omba mfanya kazi wa huduma kwa nakala ya rasilimali hii

Majibu kwa Maswali yanayoulizwa zaidi kuhusu HIV/AIDS

Simu za habari za HIV

[www.sesiahs.health.nsw.gov.au/
albionstcentre/documents/pdfdocs/HIV_FAQ_Booklet_August_2006.pdf](http://www.sesiahs.health.nsw.gov.au/albionstcentre/documents/pdfdocs/HIV_FAQ_Booklet_August_2006.pdf)

Mimi ni mja mzito, je, nahitaji kipimo cha HIV?
Inapatikana katika Kiingereza na lugha ny-
ingine

www.multiculturalhivhepc.net.au

Kupima



Wanawake na HIV: Vifurushi ya habari za mfululizo kwa wanawake kuhusu HIV
Kutungwa na FPNSW katika ubia na MHAHS, ACON na HHAS Juni 2009